Toleo 62 - Rajab 1443 AH / Machi 2021 M

# Jarida la UQAB



# Afisi Kuu ya Habari:
# Angazo la Amali za Kimataifa za Hizb ut Tahrir katika Kumbukumbu ya Kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah
# 1443 H – 2022 M




Katika mwezi wa Rajab al-Muharram mwaka huu 1443 H - 2022 M, na kwa mnasaba wa kumbukumbu chungu ya wahalifu kuiondoa dola ya Kiislamu na kukomesha nidhamu ya utawala wa Kiislamu (Khilafah) mnamo tarehe 28 Rajab al-Muharram 1342 H sawia na 03/03/1924 M, Hizb ut Tahrir inaandaa amali pana za umma katika nchi zote inamofanyia kazi, na sisi katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika ukurasa huu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu tutaangazia kwa kina amali hizo, tukimuomba Mwenyezi Mungu (swt) aharakishe kusimamisha Dola ya Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume, na Mwenyezi Mungu ni muweza wa hilo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema katika yale aliyoyapokea Imam Ahmad katika Musnad yake:

**"تكون النبوة فيكم ما شاء الله أن تكون، ثم يرفعها الله إذا شاء أن يرفعها، ثم تكون خلافة على منهاج النبوة فتكون ما شاء الله أن تكون، ثم يرفعها الله إذا شاء أن يرفعها، ثم تكون ملكًا عاضًا فيكون ما شاء الله أن يكون، ثم يرفعها إذا شاء الله أن يرفعها، ثم تكون ملكًا جبرية فتكون ما شاء الله أن تكون، ثم يرفعها الله إذا شاء أن يرفعها، ثم تكون خلافة على منهاج النبوة، ثم سكت".**

**"Utume utakuwepo kwenu kwa muda apendao Mwenyezi Mungu uwepo, kisha atauondoa apendapo kuuondoa. Kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume, na itakuwepo kwa muda apendao Mwenyezi Mungu iwepo kisha ataiondoa apendapo kuiondoa. Kisha utakuwepo utawala wa kurithishana, utakuwepo kwa muda apendao Mwenyezi Mungu uwepo kisha atauondoa apendapo kuuondoa. Kisha utakuwepo utawala wa kutenzana nguvu, utakuwepo kwa muda apendao Mwenyezi Mungu uwepo kisha atauondoa apendapo kuuondoa. Kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume, kisha akanyamaza."**

**Ijumaa, 03 Rajab 1443 H sawia na 04 Februari 2022 M**


**Email: info@uqab.or.ke**

# Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir Chazindua Kampeni ya Kimataifa: “Khilafah: Yenye Kuhakikisha Hadhi, Usalama na Haki za Kisheria za Wanawake”

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

Mwezi wa Rajab unaashiria kumbukumbu ya kutisha ya kupotea kwa Khilafah zaidi ya miaka 100 iliyopita katika kalenda ya Hijri. Dola hii inayoongoza inayotawala kwa Uislamu siku zote ilisimama kama mlinzi wa hadhi, usalama na haki za kisheria za wanawake katika ardhi za Kiislamu na kwengineko. Kufuatia kuanguka kwa Khilafah, maisha ya wanawake katika eneo hili na wanawake wa Kiislamu kote duniani yaligubikwa na aina zote za ukandamizaji na dhulma, mateso na ufukara chini ya mifumo na tawala zilizobuniwa na mwanadamu – kuanzia tawala za kidemokrasia hadi za kidikteta - ambazo zilivunja heshima yao, kushindwa kuwapa usalama wa kimwili na wa kifedha, na hazikujali chochote kuhusu haki zao za kisheria walizopewa na Mungu. Ukataji tamaa na kutapatapa vikawa ndio hadithi ya maisha yao kwa kukosekana kivuli na ulinzi unaotolewa na Sheria na Mfumo wa Mwenyezi Mungu (swt).

Kuna njia ya kutoka katika jinamizi hili hai ambalo mamilioni ya wanawake wa Kiislamu wanakabiliana nalo kote duniani, na hiyo ni kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume ambayo Mtume (saw) aliitaja kuwa ni walinzi na ngao ya Waislamu. Hata hivyo, kuna hofu nyingi, mashaka na maswali leo kuhusu dola kama hiyo inamaanisha nini kwa wanawake na hadhi na haki zao. Hofu na mashaka hayo yanatokana na uwongo wa karne nyingi, upotoshaji na mashambulizi ya serikali za kikoloni za Magharibi, waandishi, vyombo vya habari na watetezi wa haki za wanawake kuhusiana na jinsi wanawake wanavoamiliwa chini ya utawala wa Kiislamu unaoendelea kuenezwa hadi leo. Hadithi na uwongo huo ziliundwa kwa makusudi na kuenezwa na watawala wa kikoloni mtawalia na wafuasi wao ili kuiangamiza Khilafah na baadaye kuzuia kurudi kwake, kwa lengo la kudumisha na kuendeleza ushawishi wao wa kikoloni na udhibiti wa siasa na rasilimali za ardhi za Kiislamu.

Kwa hivyo Rajab hii, Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir, kimezindua kampeni ya kimataifa ya kushughulikia hofu, mashaka, na maswali haya kuhusu hadhi ya wanawake chini ya utawala wa Kiislamu. Kampeni hii yenye kichwa, “Khilafah: Yenye Kuhakikisha Hadhi, Usalama na Haki za Kisheria za Mwanamke,” inalenga kuwasilisha ufahamu wa wazi na dira ya jinsi maisha ya halisi yatakavyokuwa kwa wanawake chini ya kivuli cha dola ya Khilafah kuhusiana na haki zao, dori na muamala kama inavyothibitishwa na nususi za Kiislamu, na kudhihirishwa na utawala wa Kiislamu huko nyuma, mbali na uwongo na upotoshaji wa wasomi wa mashariki na wa kikoloni. Muhimu zaidi, tutajaribu kueleza jinsi kanuni, sheria, taasisi, miundo na nidhamu za Khilafah zitaweza kutatua kivitendo matatizo mengi ya kisiasa, kiuchumi, kimahakama, kielimu, kiafya na kijamii ambayo wanawake wanakabiliana nayo leo na kwamba mifumo yote iliyotungwa na mwanadamu, ikiwemo demokrasia - Mashariki na Magharibi - imeshindwa kutatua.

Tunatumai kwamba mtafuatilia na kuunga mkono kampeni hii muhimu inayolenga kufuta uwongo, kuvunja khofu, na kuwasilisha ukweli wa nafasi ya wanawake chini ya Khilafah ili tuweze kugeuza kukata tamaa kuwa matumaini na kusimamisha dola ambayo itamaliza jinamizi lililo hai linalowatesa mamilioni ya wanawake leo na kujenga mustakabali angavu, wenye uadilifu zaidi, salama na wenye hadhi kwa wanawake wa Umma huu wa Kiislamu.

**﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾**

**“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.” [An-Nur: 55]**

**#YenidenHilafet #ReturnTheKhilafah #الخلافة_101 #أقيموا_الخلافة**

**#TurudisheniKhilafah**


Email: info@uqab.or.ke

# HABARI NA MAONI
# Khilafah Itawalinda Wanawake Dhidi ya Ukatili Sio Upitishaji wa Sheria za Kisekula

**Habari:**

Rais wa Amerika Joe Biden mnamo Jumatano, 9 Februari 2022 alitoa taarifa kwa kichwa, “Taarifa ya Rais Biden kuhusiana na Utangulizi wa Uidhinishaji Upya wa Sheria ya 2022 ya Kupambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake.” Alihitimisha taarifa yake kwa kusema kwamba, “Kupambana na ukatili wa kinyumbani, unyanyasaji wa kingono, ukatili wa kuchumbiana na uviziaji hautakiwi kuwa ni suala la chama cha Kidemokrasia au Kijamhuri. Ni jambo la haki na kuhurumiana. Nashukuru sana kutokana na mswada huu muhimu ulioleta pamoja vyama viwili unasonga mbele, na natarajia kuwa Bunge litauidhinisha na kuuweka mezani kwangu haraka upesi.” *White House*

**Maoni:**

Sheria inayopambana na Ukatili Dhidi ya Wanawake iliandikwa kwa mara ya kwanza na kupigiwa upatu na Rais Biden pale alipokuwa Seneta na kupitishwa kuwa sheria mnamo 1994. Sheria hiyo imerekebishwa takribani mara tatu ili kuzingatia hali iliyoko sasa na maslahi mapya. Ni kinaya kwamba Amerika inajipiga kifua kama ndio mwanga wa demokrasia, lakini inataabika kindani kutokamana na kujisalimisha kwake kwa mfumo wa kirasilimali wa kisekula. Ni muhimu kutambua kwamba mzizi wa misukosuko inayowakabili wanawake na jamii kwa ujumla sio kwa sababu sheria hazijakazwa. Alas! Ni natija ya wanadamu kujitwika nguvu za Muumba, Allah (swt) katika utungaji wa sheria.

Haijalishi ni sheria ngapi zimepitishwa, hazitotatua matatizo ambayo taifa la kisekula inakabiliwa nayo pasina kuzingatia ni Amerika, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Uchina, Urusi, n.k. kwa sababu zote zimeasisiwa juu ya itikadi batili ya kisekula. Haishangazi kuona takwimu zikithibitisha hali ya kutamausha iliyoenea duniani. Kwa mujibu wa utafiti wa hivi karibuni wa nchi hatari zaidi duniani kwa wanawake unaiweka Amerika Na..19! Kwa upande mwingine, nchi kubwa ya kidemokrasia, India kuwa Na.9! *World Population Review*

Tiba ya maradhi haifanywi kwa kubahatisha kwa kumuangalia tu mgonjwa na kupendekeza matibabu fulani. Bali, mgonjwa hulazimika kufanyiwa ukaguzi wa kina ili kuweza kutambua na kuwa na yakini kile kinachomsibu mgonjwa. Kufikia sasa wanawake (feminists) na wanaume (manginas) wanaodai kulingania kumwezesha na kumkomboa mwanamke pamoja na mashirika yao ya kieneo na kimataifa wamekata tamaa katika mapambano yao hadaifu. Hii ni kutokana na juhudi zao zimeambulia patupu kwa kuwa nidhamu za kirasilimali za kisekula zilizopo ambazo zipo zinapigia debe udhalilishaji na kuwafanya wanawake kama chombo cha ngono.

Mfumo wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zinazochipuza kutokamana nazo kama vile nidhamu huria ya kijamii ambayo imepelekea ukandamizaji wa wanawake na kusambaratika kwa familia na uwiano wa kijamii; ni maradhi ya muda mrefu ambayo yamepenya katika kila Nyanja ya maisha. Hivyo basi, ni dharura kupatikane suluhisho mbadala ili kuweza kuwanusuru wanawake na jamii kwa ujumla kutoka katika dhiki zinazozidi kila kukicha. Naam! Mbadala unahitajika kwa sababu hivi sasa tumevuka zama za kujaribu na kukosea ambapo akili ya mwanadamu imeganda kifikra licha ya kwamba kiuhalisia anaonekana kuwa hai na anapumua!

Mbadala ni Khilafah, nidhamu ya utawala wa Kiislamu ambayo inaongozwa na mwanamume Muislamu, mtawala Khalifah. Khilafah imeasisiwa juu ya Shari’ah ya Kiislamu na sio uwerevu wa mwanadamu kama vile mifumo ya kirasilimali na kikomonusti na nidhamu zao na tawala zao. Kukosekana kwa Khilafah kwa zaidi ya miaka 101 Hijria tangu kuvunjwa kwake mnamo 28 Rajab 1342 imepelekea dunia kujaa mahangaiko na majanga yasiyoingia akilini yenye kuendelea yakiondosha matumaini ya utulivu na ustawi wa kweli.

Hatima yake, ni kuwa juhudi zinatakiwa kuelekezwa katika kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume. Kurudi kwa Khilafah kutawahakikisha wanawake na jamii kwa ujumla kupata hadhi, usalama na haki za Kishari’ah. Khilafah itakuwa ni mlinzi na ngao kwa walio madhaifu na nguvu pasina kuzingatia dini au hali zao za kijamii na kiuchumi. Kurudi kwake kutadhamini furaha na ustawi wa kweli.

**وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ “Na siku hiyo Waumini watafurahi.” [Ar-Rum 30: 4].**

**Imeandikwa kwa ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# HABARI NA MAONI
# Uislamu ndio Wokovu Pekee kwa Watoto wa Tharparkar

**Habari:**
Ripoti ya kuogofya ya vifo vya watoto zaidi ya 36 katika wilaya ya Tharparkar, vilivyosababishwa na maradhi mbalimbali katika mwezi wa kwanza wa 2022, imesababisha kizungumkuti kwa serikali ya mkoa. (Tribune Pakistan)

**Maoni:**
Kwa mujibu wa rekodi ya Idara ya Afya ya Tharparkar, zaidi ya watoto 600 waliozaliwa walikufa katika mwaka uliotangulia, 2021. Vifo hivi vilitokana haswa na kutopatikana kwa huduma za afya na lishe duni. Kama tunavyojua sote kwamba maisha yanategemea maji, watu wa Thari hutumia sehemu kubwa ya siku yao kutafuta maji safi ya kunywa, na katika hili, usafi wao ni tofauti na usafi wa kawaida.

Kuna vyanzo tofauti wanavyotumia, kama kukusanya maji ya mvua na visima virefu vilivyochimbwa. Kwa sababu ya matumizi ya mara kwa mara ya maji ya ardhini yenye floridi ya juu, maradhi ya fluorosis yamekuwa janga eneo la Thar, na kusababisha fluorosis ya meno, ulemavu wa viungo, na matatizo ya tezi na figo. Hii inasababisha watu wazima wenye utapiamlo kuzalisha na kulea (kama watabakia hai) watoto wenye utapiamlo. Wilaya ya Tharparkar ina wakazi wanaokadiriwa kuwa milioni 1.6, waliosambaa zaidi ya kilomita 22,000 mraba. Uhaba wa maji ni tatizo kubwa la eneo hili. Na visima vilivyochimbwa vimepatikana kuwa chanzo pekee endelevu cha maji ya ardhini. Wamekuwa wakiishi kwa maji yaliyochafuliwa, chumvi na maji ya ardhini ambayo hayajatibiwa. Siku yao huanza kwa kubeba mitungi ya maji, ambayo hujaza kutoka kwa maji ya mvua yaliyohifadhiwa au matangi madogo ya asili, baada ya kutembea zaidi ya kilomita 3 kwenye joto kali.

Serikali tofauti tofauti kwa miaka mingi zimetumia kisiasa ukame, njaa na vifo vya watu wa Thari kwa manufaa yao wenyewe. Miradi ya maji ilitangazwa ambayo haikufikia kukamilika; kutokuwepo kwa vituo vya matibabu huongeza mafuta kwenye moto na kutafuta msaada wa matibabu kunaweza kuwagharimu watu wanaolazimika kutembea umbali mrefu na kutumia pesa nyingi. Mnamo 2021, Mahakama ya Upeo iligundua vifo vya watoto, na iliona kuwa hakuna madaktari, dawa au vituo vya afya vilivyopatikana katika hospitali za Tharparkar, ambayo inaonyesha kukatika kabisa mafungamano ya Serikali na watu.

Watu wa Ummah huu wanahisi uchungu kwa kaka na dada zao na tunaona watu binafsi na mashirika mengi yakifanya kazi kwa ajili ya watu wa Thari. Kambi za matibabu za kibinafsi zimewekwa na watu na msaada pia hutolewa lakini bila shaka hizi haziwezi kukidhi mahitaji. Kwa njia hii watu huishia kulipa gharama mara mbili, kwanza kwa Serikali kwa njia ya kodi na pili kwa kuwasaidia watu wa Thari moja kwa moja. Suala hili linahitaji mpango ufaao na haliwezi kusuluhishwa, Tharparkar ndio jangwa pekee lenye rutuba duniani na kwa mujibu wa uchunguzi wa kijiolojia wa hifadhi ya makaa ya mawe ya Pakistan inakadiriwa kuwa takriban tani bilioni 175, na kuifanya kuwa mojawapo ya hifadhi kubwa zaidi za makaa ya mawe ya lignite Dunia. Endapo hifadhi hizi zitatumiwa kwa uaminifu basi sio tu zinaweza kusaidia kutatua matatizo ya nishati ya Pakistan, vilevile zinaweza kupanga maisha ya utu kwa watu wa Thari. Hata kama hakukuwa na hifadhi ya makaa ya mawe, na kutengeneza mifereji ya maji kwa ajili ya kuwasaidia watu wa Thar haikuwezekana, jukumu la Serikali la kuokoa maisha na riziki za watu wake bado linabakia.

Katika Uislamu, Mtawala ni mmoja kwa Ummah mzima wa Kiislamu, bila kujali rangi au eneo la makaazi. Ni chini ya kivuli cha Khilafah pekee, ndipo tutaona afueni kwa Ummah katika nyanja zote za maisha. Mali za umma zitatumika kwa manufaa ya umma. Khalifah atateua magavana na hao magavana watawajibika kwa eneo lao. Khalifah mwenyewe atafuata mtindo wa Khalifah Umar Bin Al-Khattab aliyeongoka, ambaye kipindi chake cha utawala kilikuwa kirefu zaidi kati ya Makhalifa Waongofu wanne wa mwanzo. Alijulikana sana kwa hisia zake kali za uwajibikaji katika kushughulikia mambo ya Waislamu. Alifanya doria usiku ili kuhakikisha watu wanatunzwa vyema. Mwenyezi Mungu atujaalie mtawala muadilifu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

مَا مِنْ عَبْدٍ يَسْتَرْعِيهِ اللَّهُ رَعِيَّةً يَمُوتُ يَوْمَ يَمُوتُ وَهُوَ غَاشٌّ لِرَعِيَّتِهِ إِلَّا حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ

“**Hakuna mja yeyote ambaye Mwenyezi Mungu anamfanya msimamizi wa raia kisha akafa ilhali anawaghushi raia wake, isipokuwa Mwenyezi Mungu amemuharamishia Pepo.**” [Al-Bukhari na Muslim]. Riwaya nyengine ni: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

«فَلَمْ يَحُطْهَا بِنُصْحِهِ لَمْ يَجِدْ رَائِحَةَ الْجَنَّةِ» “**Kisha asiangalie mambo yao kwa wema na ikhlasi, hatanusa harufu ya Pepo.**” Riwaya ya Muslim ni: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

مَا مِنْ أميرٍ يلي أمور المُسْلِمينَ، ثُمَّ لا يَجْهَدُ لَهُمْ وَيَنْصَحُ لَهُمْ، إِلاّ لَمْ يَدْخُلْ مَعَهُمُ الْجَنَّةَ

**“Hakuna kiongozi yeyote, anayetawala mambo ya Waislamu, asijizatiti kwa ajili yao na asiwatumikie kwa ikhlasi, isipokuwa hataingia pamoja nao Peponi.”**


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ikhlaq Jehan**




**Email: info@uqab.or.ke**

Afisi kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 22/1443 Jumatatu, 28 Jumada II 1443 H 31/01/2022 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Warohingya Wakimbia Moto hadi Motoni; Ni Dola ya Khilafah pekee Ndio Itakayowaokoa na Kuwaregeshea Haki zao

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) liliripoti moto mkali katika kituo cha matibabu cha COVID-19 katika kambi ya Cox's Bazar nchini Bangladesh, ambayo huhifadhi wakimbizi wanaokimbia kutoka Myanmar, mnamo Jumapili alasiri, 9/1/2022. Shirika hilo la Umoja wa Mataifa lilisema, katika ukurasa wake wa Twitter, kwamba hakuna aliyejeruhiwa kutokana na moto huo uliozuka, lakini lilibainisha kuwa moto huo uliathiri maelfu ya wakimbizi wa Rohingya, na kusababisha uharibifu mkubwa kwa sehemu za kambi hiyo kubwa zaidi ya wakimbizi katika duniani, ambayo inajumuisha karibu wakimbizi 900,000.

Kambi ya Cox's Bazar imeundwa kwa vijumba vya mianzi na turubai, na kuifanya iwe rahisi kushika moto, na kuongeza mateso na hofu ya wakimbizi.

Ikumbukwe kwamba hii si mara ya kwanza kwa kambi hii kukabiliwa na hatari hii na nyinginezo. Mnamo Machi 2021, nyumba 10,000 zilichomwa moto na angalau watu 45,000 walilazimika kuyahama makaazi yao. Mafuriko makubwa ya monsoon mnamo Julai 2021 yaliathiri wakimbizi 46,000 na kusababisha maporomoko makubwa ya ardhi.

Ndugu na dada zetu walikimbia kutokana na uonevu wa wahalifu wa Myanmar. Walikabiliwa na vita vya kikabila kwa kuchomwa moto vijiji, kuuawa na kunyanyaswa; jambo ambalo mamlaka ya Myanmar inakanusha, ikidai kuwa wanapambana na Waislamu wenye misimamo mikali. Kwa hakika, inatafuta, pamoja na chuki na uadui wake kwa Uislamu na Waislamu, kuwaangamiza watu hawa na kuwaritadisha waliosalia kutoka kwenye Dini yao.

Ndugu na dada zetu walikimbia kifo, wakitumaini kuokoka na kuishi kwa usalama, lakini serikali ya Bangladesh haikuwapa hilo, kwa hiyo wakawa kama wale waliotafuta kimbilio dhidi ya joto kali ndani ya moto! Wanaishi katika nyumba zinazotishiwa na moto unaoteketeza nguo zao na mianzi, na hauwalindi kutokana na baridi na mafuriko ya msimu wa baridi. Ni nyumba, kama ambaye si nyumba! Ni kuwahadaa tu watu, kwani serikali hii haifurahii uwepo wao katika ardhi yake, na mara nyingi imeeleza kuwa ina nia ya kuwafukuza na kuwaregesha Myanmar, licha ya hatari ya maisha yao, haswa baada ya kampeni kikatili ya kijeshi iliyoanza dhidi yao mnamo Agosti 2017, ambayo iliwafanya watishiwe na kutokuwa salama.

Hali ya wakimbizi Waislamu nchini Bangladesh na kwingineko inadhihirisha njama za serikali zilizopo katika nchi za Kiislamu pamoja na maadui wa Waislamu. Wakimbizi hawa walizikimbia nchi zao kwa kuogopa kifo, wakituhumiwa kwa misimamo mikali na ugaidi, kuishi maisha ya unyonge na ukandamizaji katika nchi walizokimbilia. Walipoteza usalama, utulivu, na makao. Walikimbia kuokoa maisha yao, wakitumaini kwamba watapata hifadhi katika serikali hizi, lakini matumaini yao yalikatika na moto walioukimbia ukawafuata, na hofu, kupuuzwa na kifo kikawafuata.

Enyi Umma wa Kiislamu: Hawa ni kaka na dada zetu, ambao walidhulumiwa na wahalifu. Wakawahamisha, wakawatiisha, na wakawadhoofisha, hivyo wakakimbia pamoja na Dini yao wala hawakuibadilisha. Walitafuta usalama katika serikali hizi, lakini walikatishwa tamaa. Je, kimbilio hutafutwa kutoka kwa watu kama hao?! Ni vibaraka wanaofuata upotofu wa wahalifu na mbinu zao na wanashirikiana nao kuwagandamiza Waislamu na kuipiga vita Dini yao.

Enyi Umma wa Kiislamu: Hawa ni ndugu zetu wanaoteseka, basi unyonge huu utaendelea hadi lini? Mpaka lini maadui wa Mwenyezi Mungu watawakandamiza watoto wenu na hali nyinyi mmenyamaza kimya? Basi inukeni na mkukute vumbi la udhalilishwaji kutoka kwenu, naapa kwa Mwenyezi Mungu, hili halikubaliki kwenu, kwa sababu Mwenyezi Mungu (swt) amewafanya kuwa Umma bora uliotolewa kwa watu.

*Endelea... UK 7*

Sisi katika Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir tunatoa wito kwa kila mwenye ikhlasi kutoka kwa watu wenye nguvu na ulinzi kunusuru ulinganizi wetu wa kuregesha hukmu kwa yale yote aliyoteremsha Mwenyezi Mungu (swt) na kuregesha Dola ya Khilafah ambayo kwayo peke yake dhulma itaondolewa kutoka kwa kila Muislamu mwanamume na mwanamke na kutoka kwa wote wanaoishi chini ya kivuli chake. Tunawalingania wanachuoni wa Umma huu kunusuru neno la Mwenyezi Mungu ili liwe juu, kutekeleza wajibu wao. Enyi warithi wa Mitume, rekebisheni hali ya Ummah wenu na pazeni sauti zenu dhidi ya watawala wenu, linganieni umoja wa Ummah wenu na kurudi kwa mamlaka yake.

Tunamuomba kila Muislamu mwanamume na mwanamke kufanya kazi pamoja nasi katika kuinusuru Dini hii na kuifanya kuwa yenye kutawala duniani ili tuwanusuru ndugu zetu kila mahali.

Hatutawaondolea dhulma na ukandamizaji, udhalilifu na umasikini wanaoupata, isipokuwa dola isimamishwe upya kwa ajili ya Waislamu inayowahami na kuwaepusha na kila uvamizi.

Tuwamuomba Mwenyezi Mungu (swt) aviunganishe viungo vilivyotawanyika vya Umma huu, aunusuru, na aregeshe utukufu na fahari yake haraka zaidi.

(وَكَانَ حَقّاً عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِينَ)

**“...Na ilikuwa ni haki juu yetu kuwanusuru Waumini”** [Ar-Rum: 47]

**Kitengo cha Wanawake**
**katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Ni Khalifah Pekee Anayejibu Mahitaji ya Wanawake wa Kiislamu

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Zehra Malik**



Ushauri (Shurah) na kuhisabu zote ni amri za Mwenyezi Mungu (swt), na miongoni mwa kanuni za hukmu ya Kiislamu, na ni wajibu kwa Khalifah. Kuaminiana kati ya mtawala na raia wake kunahakikishwa kupitia mtawala kuchukua ushauri na mtawala kuhesabiwa na raia wake. Hata hivyo, kwa kuondolewa kwa Khilafah, Waislamu wamenyimwa chanzo hiki cha nguvu, uaminifu na mamlaka. Kito chetu hiki, kilibadilishwa kwa nidhamu duni, mbovu na potofu inayoitwa demokrasia, iliyozaliwa na akili fisadi. Chaguzi za kidemokrasia na mabunge zilidaiwa kuwa zinatokana na Uislamu, zikifananisha na hukmu ya Kiislamu ya Shurah na uwajibikaji. Walidai kuwa mwanamke wa Kiislamu alionewa, alinyamazishwa na kuchukuliwa kuwa ni sehemu isiyo na natija katika jamii katika karne za Khilafah. Badala yake walimuahidi kuwa na ufanisi na ushawishi katika kuunda nchi zao, watu na ulimwengu kwa njia ya demokrasia ya Kimagharibi.

Hakika, tunaona kwamba wanawake wachache wa Kiislamu, wanaoinuka kuzungumza kwa neno "demokrasia" wakilingania fikra na mifumo ya Urasilimali, wanapewa haki ya kuzungumza katika nchi za Kiislamu, katika Umoja wa Mataifa, katika vyombo vya habari na mabunge ya Amerika au nchi yoyote ya kibepari yenye uadui na Uislamu. Waliweka kundi la watu wasio na akili na wasio na utu karibu nao ili kuunda udanganyifu kana kwamba wanaweza kushawishi watu. Kiasi kwamba hata wao wenyewe wanashangazwa na taswira yao halisi. Jambo kuu ni, wakati baadhi ya wanawake hawa wa Kiislamu wa kidemokrasia wanapewa nyadhifa, vyeo, na tuzo, na kuonyeshwa kama wanawake imara na wenye vivumishi kama vile "mwanamke wa mwaka, watu 100 wenye ushawishi mkubwa zaidi duniani" kwenye jalada la majarida na kusifiwa kama vielelezo, wanaamini kuwa wamepata mafanikio ya kweli. Lakini, wanachofanya ni utekelezaji wa neno moja kwa moja wa orodha ya majukumu waliyopokea na washauri wao wa Kimagharibi. Kwa hakika hotuba zao zote ziliishia kuwa hewa moto na kauli mbiu tupu, huku zikishindwa kuboresha maisha ya wanawake wa Kiislamu. Hawaoni wala hawataki kuona kuwa ni mifumo hii ya kidemokrasia ndiyo inayowanyima wanawake wa Kiislamu mamlaka na uwezo wao, na kuwakataza kupaza sauti zao kama Waislamu, badala yake inawapa nguvu wakoloni wanaosababisha matatizo baada ya matatizo. Wale wanaotenda ndani ya muundo wa mfumo wa kidemokrasia hawawezi kutimiza matakwa yoyote ya wanawake wa Kiislamu, isipokuwa kama haya yataafiki watawala na tawala zao. Ndiyo maana hatuoni kamwe watetezi wa demokrasia wakiboresha maisha ya wanawake wa Ummah huu.

Ama kwa hakika, wanawake wa Kiislamu wanaowalingania watawala wao kutawala kwa mujibu wa sheria za Kiislamu na si kwa mujibu wa demokrasia, wanaswekwa na mifumo ya sheria za kisekula, na hata kufungwa jela. Ni upotoshaji ulioje kuzungumzia uhuru na haki za kidemokrasia za wanawake, huku mabepari wa kikoloni wakiongozwa na Marekani wakivamia ardhi zetu na kuzigeuza kuwa viwanja vya vita, kuiba mali zetu na kutia sumu akili za vijana wetu kwa thaqafa zao, yote ikiwa ni kwa kisingizio cha kuwakomboa wanawake wa Kiislamu kwa demokrasia... Huku wengine

***Endelea... UK 9***

wakipongezwa kwa kutukuza demokrasia na uhuru, wanawake wa Kiislamu, wanaoyaomba majeshi ya Waislamu kuokoa heshima zao, maisha yao, ardhi zao, na wanaoulingania umoja kwa Umma wanatangazwa kuwa magaidi... Kwa hakika, wale wanawake wa Kiislamu wanaoelezea waziwazi matamanio ya wanawake wengi wa Kiislamu, na wanaodai suluhisho la matatizo yao kama inavyotarajiwa na Uislamu, hawanyimwi tu sauti kwenye vyombo vya habari vya mifumo ya kisekula ya kidemokrasia, wananyimwa haki yao ya kuzungumza na watawala wao. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa fahamu za demokrasia, "kushauri na kuhisabu" zinatumika kuasisi kila aina ya haramu, kuhujumu mfumo wa maisha ulioamriwa na Mwenyezi Mungu, na kuuondoa katika uwanja wa maisha!

Hata hivyo, chini ya utawala wa Kiislamu wa Khilafah, ambao ni aina ya utawala kama ilivyoainishwa kwa Waislamu na Mwenyezi Mungu, neno la mwanamke lina thamani halisi. Uislamu unamlazimu mtawala wa Waislamu, Khalifah, kukidhi mahitaji ya kila mwanachama wa Ummah. Kwa ajili hiyo, Yeye (swt) anamuamuru kushauriana na Waislamu na kuwawajibisha Waislamu kumhisabu mtawala wao. Katika Dola ya Khilafah, kazi hii muhimu itatekelezwa ndani ya Majlis ya Ummah. Baraza la Ummah (Majlis al-Ummah) ni mkusanyiko wa watu binafsi wanaowakilisha mambo ya Waislamu, ili Khalifah aweze kuwaregelea juu ya haya. Wawakilishi hawa huchaguliwa na Ummah ili waweze kutoa malalamiko yao kuhusiana na vitendo vya kidhalimu vinavyofanywa na watawala au matumizi mabaya ya sheria za Kiislamu. Kila raia aliyekomaa na mwenye akili timamu wa Dola, mwanamume na mwanamke, Muislamu au asiyekuwa Muislamu, ana haki ya kuwa mwanachama wa Majlis al-Ummah. Maoni na ushauri wao juu ya vitendo na mambo ya kivitendo yanayohusiana na usimamizi wa mambo ya ndani, kama vile mambo ya utawala, elimu, afya, na uchumi, viwanda, kilimo na mengineyo Khalifah anafungika nayo. Kwa hakika, pale Khalifah anapotaka maoni yao juu ya masuala haya, hana budi kuchukua maoni ya walio wengi. Katika mambo yote haya, neno la mwanamke wa Kiislamu lina nguvu sawa kwa sawa na neno la mwanamume.

Hizb ut Tahrir ilibainisha jambo hili katika maelezo yake yote katika Rasimu ya Katiba ya Dola ya Khilafah - Ibara ya 105 hadi 111 - pamoja na dalili zake za Kiislamu. Wanawake wa Kiislamu wataweza tu kueleza mawazo na hisia zao za Kiislamu, na mahitaji yao, na kudai vitendo kwa mujibu wa radhi za Mwenyezi Mungu (swt) ndani ya mfumo wa Kiislamu, unaotabikishwa chini ya Khilafah. Hapo, sauti yao ndipo itapata mawasiliano ya kweli na utekelezwaji katika uwanja wa maisha, kwani itakuwa inamfunga mtawala.

Mahali pekee, ambapo tunaweza kuishi maisha yanayolingana na radhi za Mola wetu, ni Dola ya Khilafah. Ni Dola ya Khilafah tu, ambapo tunaweza kuwa kina mama, wake, mabinti, na wanasiasa wenye ushawishi mkubwa. Mfumo mwengine wowote huwalaani wanawake wa Kiislamu na wasiokuwa wa Waislamu kwa kuwaweka hatarini ya ukatili unaotokana na akili na matamanio ya wanadamu.

أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ

**"Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini?" [Surah al-Maidah: 50].**

**#YenidenHilafet** **#ReturnTheKhilafah**
**#الخلافة_101** **#أقيموا_الخلافة**

**#TurudisheniKhilafah**





Email: info@uqab.or.ke












Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

Angazo la Amali za Kimataifa za Hizb ut Tahrir

katika Kumbukumbu

ya Kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah

1443 H – 2022 M

Angazo la Amali za Kimataifa za Hizb ut Tahrir Katika Kumbukumbu ya Kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah 1443 H – 2022 M

الخلافة

Khilafah

#ReturnTheKhilafah #YenidenHilafet #أقيموا_الخلافة

www.hizb-ut-tahrir.info


Email: info@uqab.or.ke











## Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

## Angazo la Amali za Kimataifa za Hizb ut Tahrir katika Kumbukumbu ya Kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah 1443 H – 2022 M

Angazo la Amali za Kimataifa za Hizb ut Tahrir Katika Kumbukumbu ya Kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah 1443 H – 2022 M

الخلافة
Khilafah

#ReturnTheKhilafah #YenidenHilafet #أقيموا_الخلافة

www.hizb-ut-tahrir.info


Email: info@uqab.or.ke

# KENYA










**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Angazo la Amali za Kimataifa za Hizb ut Tahrir katika Kumbukumbu ya Kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah**

**1443 H – 2022 M**

Angazo la Amali za Kimataifa za Hizb ut Tahrir

الخلافة

Khilafah

Katika Kumbukumbu ya Kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah 1443 H – 2022 M

#ReturnTheKhilafah #YenidenHilafet #أقيموا_الخلافة

www.hizb-ut-tahrir.info

 Email: info@uqab.or.ke